

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TISA**

**KIKAO CHA KUMI**

**11 NOVEMBA, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TISA

**KIKAO CHA KUMI – TAREHE 11 NOVEMBA, 2022**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA AFYA:**

Maelezo ya Waziri wa Afya kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hati ya Uhamisho wa Bajeti baina ya Mafungu Na.1 kwa Mwaka 2021/2022 [*Statement of Reallocation Between Votes – Reallocation Statement No.1 of 2021/2022*].

Hati ya Uhamisho wa Bajeti Ndani ya Mafungu Na.2 kwa Mwaka 2021/2022 [*Statement of Reallocation within Votes - Reallocation Statement No.2 of 2021/2022*].

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

#### **139. MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali haioni haja ya kuzungumza na Taasisi za Kifedha ili mikopo kwa Watu Wenye Ulemavu itolewe kwa mtu mmoja mmoja.

#### **140. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, kuna mpango gani wa kutoa mwongozo wa upandishaji mishahara kwa Wafanyakazi wa Sekta Binafsi.

#### **141. MHESHIMIWA ZAINABU ATHUMAN KATIMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini marekebisho ya Sheria yataletwa ili Mwanamke anayejifungua Mtoto njiti aongezewe likizo ya uzazi.

## **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

### **142. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni nini kinakwamisha barabara ya Magamba, Mtapenda, Kasokola hadi Ifukutwa kuhamishiwa TANROADS.

### **143. MHESHIMIWA SHAMSIA AZIZI MTAMBA (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza vipimo vya Maabara hasa vya Malaria katika Zahanati za Mtwara Vijijini.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **144. MHESHIMIWA ASYA SHARIF OMAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini changamoto ya usafiri katika Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba itatatuliwa.

## **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

### **145. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Sheria ya kuweka ukomo wa upelelezi kwenye kesi za mauaji nchini.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **146. MHESHIMIWA ELIBARIKI IMMANUEL KINGU (SINGIDA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Singida hadi Sepuka kuelekea Kizaga Wilaya ya Ikungi itajengwa kwa kiwango cha lami.

### **147. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, nini hatma ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Geita - Nyarugusu - Kahama hasa kipande cha Geita - Nyarugusu – Bulyanhulu.

**148. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni Sheria gani inayotumika kwenye tozo za Bandari nchini.

**WIZARA YA NISHATI:**

**149. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO  
(MPANDA VIJILI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaa Kingaradi katika eneo la Mwese lenye milipuko ya radi mara kwa mara.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**150. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI  
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA Wilayani Busega.

**151. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU  
(TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,  
Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA  
Wilayani Tunduru.

**WIZARA YA MADINI:**

**152. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

- Je, kuna mkakati gani kuiwezesha GST kufanya utafiti wa kisayansi na teknolojia kuhusu *Critical Minerals* ili kudhibiti mabadiliko ya hali ya hewa.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**153. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI  
MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,  
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, kuna mpango gani wa kuboresha minara ya  
mawasiliano ya simu katika Kata za Makurunge  
na Fukayosi.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **154. MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini skimu za umwagiliaji Ukanda wa joto Ihowanza, Malangali, Idunda, Mbalamaziwa, Itandulu, Nyololo na Maduma zitajengwa.

## **WIZARA YA AFYA:**

### **155. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha huduma za afya zikiwemo dawa muhimu katika Hospitali zetu.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **156. MHESHIMIWA TABASAM HAMIS MWAGAO (SENGEREMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itawavuna Tumbili katika Kisiwa cha Juma Wilayani Sengerema ambao wanakula mazao ya Wananchi.



**157. MHESHIMIWA DAUD PROTAS VENANT  
(IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani wa kugawa baadhi ya maeneo ya Hifadhi Igalula kwa Wananchi ili wapate maeneo ya kuchungia na makazi.

**IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima  
na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022.

**V. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:**

**VI. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:**

**WAZIRI MKUU:**

**VII. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA  
MASHARIKI:**

**DODOMA  
11 NOVEMBA, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**